ISSN 2820-2686 | Toleo la Kumi na Mbili | Julai - Septemba, 2024

# JARIDA LA WAKILI MKUU

## OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI YAPATA WAKILI MKUU MPYA



## DKT. ALLY POSSI
WAKILI MKUU WA SERIKALI

# BODI YA UHARIRI

## Mwenyekiti

**Alice Edward Mtulo**
Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

## Mhariri Mkuu

**Prisca Jackson Ulomi**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

## Waandishi wa Jarida

**Prisca Jackson Ulomi**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**Dennis Julius Buyekwa**
Afisa Habari

## Msanifu wa Jarida

**Nyamhoni Robert Chacha**
Afisa TEHAMA

## Wajumbe

**Saddy Rashid Sevingi**
Mkurugenzi Msaidizi Usuluhishi wa Nje

**Hangi Matekeleza Chang'a**
Mkurugenzi Msaidizi Katiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi

**Kiuye Mbwana Shemakame**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Maktaba na Utafiti

**ACPA Devota Mathew Ngulugulu**
Mhasibu Mkuu

**Mercy Rowland Kyamba**
Mkurugenzi Msaidizi - Udhibiti Ubora

**Zuhura Mohamed Kussaga**
Mchumi Mwandamizi

# TAHARIRI

**Prisca Jackson Ulomi**
Mhariri Mkuu



Tarehe 14 Agosti, 2024 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alimteua Dkt. Ally Possi kuwa Wakili Mkuu wa Serikali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alikuwa mwanzilishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mwaka 2018 akiwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, karibu tena!

Natumia nafasi hii, kumpongeza Dkt. Possi kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kushika nafasi hii muhimu ya uongozi na tunaamini kwamba atasimamia umoja na mshikamano uliopo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ili kuhakikisha malengo ya Ofisi yanafikiwa kwa wakati.

Baada ya pongezi, naomba kutumia fursa hii kumtakia kheri na fanaka Dkt. Ally Possi, Wakili Mkuu wa Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake mapya ya kuiongoza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuzingatia ujuzi, umahiri na weledi katika kusimamia masuala ya kisheria ndani na nje ya nchi. Kongole kwa Dkt. Possi!

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ikiwa na jukumu la msingi la kusimamia na kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake katika muktadha wa kutetea na kulinda maslahi mapana ya Taifa na kuiletea nchi maendeleo na kuimarisha utawala bora unaozingatia msingi wa sheria hatua itakayoendelea kuvutia wawekezaji wengi zaidi wa ndani na nje ya nchi.

Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali tunamshukuru Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumteua kiongozi makini na mzalendo Dkt. Ally Possi na tuna matumaini makubwa kwa kuwa tunaamini kuwa Ofisi hii itaendelea kuchangia kwa kiwango kikubwa katika kuimarisha na kulinda maslahi ya Taifa kupitia usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi ili kuhakikisha Serikali inaendelea kushinda mashauri mbalimbali yaliyofunguliwa ndani na nje nchi ili fedha zitakazo okolewa zielekezwe kwenye miradi mikubwa ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa nchini ili kuhakikisha Ofisi inaunga mkono juhudi za Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuwaletea wananchi maendeleo kupitia Sekta ya Elimu, Afya na Miundombinu.

Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali tuna imani kubwa na Dkt. Possi kwa azma yake ya kuboresha mazingira ya kazi yanayotoa msukumo mpya wenye ari, umoja, mshikamano na utendaji uliotukuka. Pia, ni kiongozi mwenye maono na dhamira thabiti ya kuweka mazingira wezeshi yatakayoongeza chachu kwa watumishi kuchapa kazi kwa ufanisi na uadilifu zaidi. Kwa kujenga mazingira bora na kutoa nyenzo stahiki kwa watumishi, tunaamini kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itaweza kupiga hatua zaidi kwa kushirikiana na wadau katika kuboresha huduma kwa wananchi na kuimarisha uendeshaji wa mashauri.

Kwa niaba ya Wajumbe wa Bodi ya Uhariri wa Jarida la Wakili Mkuu, ninaungana na wadau wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Sekta ya Sheria na wananchi kumpongeza Dkt. Possi kwa uteuzi huu. Tunamuombea mafanikio mema na tunatarajia kuona Sekta ya Sheria hususan Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ikipiga hatua zaidi katika uendeshaji wa mashauri ya Serikali na taasisi zake ndani na nje ya nchi. Hongera sana Dkt. Possi.

Kazi iendelee!

# Kutoka Kwenye Dawati la Mwenyekiti wa Bodi ya Uhariri



Alice Edward Mtulo
**Naibu Wakili Mkuu wa Serikali**

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya na uhai. Kipekee napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali. Natambua dhamana hii kubwa ya uendeshaji wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, naahidi kutumikia nafasi hii kwa weledi na uadilifu kwa kuzingatia matumizi bora ya rasilimali ili kuleta mabadiliko chanya yenye tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi kwa maslahi mapana ya taifa.

Kwa namna ya pekee, naendelea kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani kubwa aliyoendelea kutuonyesha kwa kumteua Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi. Tunaahidi kufanya kazi kwa juhudi, uwazi na weledi wa hali ya juu ili kutimiza matarajio ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, wadau wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na wananchi kwa ujumla ili kuhakikisha tunafikia malengo tuliyojiwekea kwa wakati.

Ni dhamira yetu kufanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na wadau, watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) walioko makao makuu ya Ofisi hii pamoja na walioko kwenye Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwenye mikoa 17 kote nchini. Mikoa hiyo ni: Dodoma, Morogoro, Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Shinyanga, Mwanza, Kagera, Mara, Mbeya, Iringa, Ruvuma, Mtwara, Rukwa, Tabora, Kigoma na Manyara.

Tunaamini kuwa kwa ushirikiano thabiti tulionao, tutaweza kufikia malengo tuliyojiwekea kwa kuhakikisha kuwa mashauri yote ya madai na usuluhishi yanaendeshwa kwa haki, uadilifu na kwa wakati kwa kuwa Ofisi imeendelea kujizatiti kwa kuimarisha mifumo na kuboresha mazingira ya kazi kwa Mawakili wa Serikali na watumishi wote wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na tija kwa ari na kwa bidii.

Tunapoelekea kipindi cha uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwezi Novemba 2024, niendelee kuwahimiza watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na wananchi wote kushiriki kikamilifu katika zoezi hili muhimu kwa kuwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni nafasi ya kuimarisha, kukuza na kuendeleza demokrasia nchini ambayo ni chachu ya ushiriki wa wananchi katika kuleta maendeleo na kujenga msingi bora wa utawala wa sheria nchini. Ushiriki wenu katika uchaguzi ni muhimu kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Niendelee kutoa wito kwa Mawakili wa Serikali kote nchini kuwa daraja la haki kwa kusimamia na kuendesha mashauri yote ya uchaguzi yatakayofunguliwa. Ni jukumu letu kama watetezi wa haki kuhakikisha kuwa tunalinda na kusimamia misingi ya sheria ili kuendeleza na kudumisha amani, utulivu na mshikamano ambayo ni tunu inayotufanya watanzania kuendelea kuwa wamoja. Kwa kuwa na msimamo huu, Tanzania itaendelea kuwa kisiwa cha amani na taifa linaloongoza kwa utulivu na mshikamano. Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Kazi Iendelee!

# Yaliyomo


UK. 06 Rais Samia Suluhu Hassan Amteua Dkt. Ally Possi kuwa Wakili Mkuu wa Serikali

UK. 12 Waziri Prof. Kabudi: Tuna Deni Kubwa kwa Watanzania

UK. 15 Waziri Dkt. Balozi Pindi Chana Aongoza Mapokezi ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria

UK. 18 Wakili Mkuu wa Serikali Akabidhiwa Ofisi

UK. 20 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Kuendeleza Ushirikiano na TLS

UK. 23 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yatoa Ushirikiano Uendeshaji Mashauri ya Serikali Mbeya

UK. 26 Menejimenti ya OWMS Yatakiwa Kuongeza Ushirikiano Katika Kutekeleza Majukumu Yake

UK. 28 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yapongezwa Songea

UK. 31 Suma JKT Yatakiwa Kuongeza Kasi Mradi wa Ujenzi Jengo la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

UK. 33 Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Atembelea Maonesho ya Sabasaba

UK. 35 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yashiriki Maonesho ya 48 ya Sabasaba

UK. 37 Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Atembelea Maonesho ya Nanenane

UK. 39 Wanafunzi wa Mafunzo kwa Vitendo Watakiwa Kufanya Kazi kwa Kutunza Siri za Serikali

UK. 41 Wakili wa Serikali Apata Tuzo ya Utatuzi wa Migogoro Kwa Njia ya Usuluhisi

UK. 43 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yaibuka Kidedea Mchezo wa Kuvuta Kamba



# UTEUZI

# Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan Amteua Dkt. Ally Possi kuwa Wakili Mkuu wa Serikali



**Dkt. Ally Possi**
*Wakili Mkuu wa Serikali*

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

*Simu: 255-262961500/1*
*Nukushi: 255-262961502*
*Baruapepe : press@ikulu.go.tz*
*Tovuti : www.ikulu.go.tz*

*OFISI YA RAIS,*
*IKULU,*
*1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,*
*CHAMWINO,*
*S.L.P 1102,*
*40400 DODOMA.*

*Dar es Salaam*
*14 Agosti, 2024*

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi na uhamisho wa viongozi mbalimbali. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Dkt. Moses Kusiluka, viongozi walioteuliwa na kuhamishwa vituo vya kazi ni kama ifuatavyo:-

**A: Uteuzi wa Mawaziri**

1. Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb.) ameteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria;

2. Mhe. William Vangimembe Lukuvi (Mb.) ameteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu);

3. Mhe. Jenista Joackim Mhagama (Mb.) ameteuliwa kuwa Waziri wa Afya. Kabla ya uteuzi huu, Mhe. Mhagama alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu); na

4. Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb.) ameteuliwa kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Kabla ya uteuzi huu, Mhe. Chana alikuwa Waziri wa Katiba na Sheria, anachukua nafasi ya Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (Mb.) ambaye ameteuliwa kuwa Mshauri wa Rais.

**B: Uteuzi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wakili Mkuu wa Serikali na Jaji wa Mahakama ya Rufani**

1. Bw. Hamza Johari ameteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kabla ya uteuzi huu, Bw. Johari alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA), anachukua nafasi ya Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi ambaye ameteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani;

1

2. Bw. Samwel Maneno ameteuliwa kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kabla ya uteuzi huu, Bw. Maneno alikuwa Msaidizi wa Rais, Sheria. Bw. Maneno anachukua nafasi ya Balozi Prof. Kennedy Gastorn ambaye ameteuliwa kuwa Mshauri wa Rais, Sheria na Mikataba; na

3. Dkt. Ally Saleh Possi ameteuliwa kuwa Wakili Mkuu wa Serikali. Kabla ya uteuzi huu, Dkt. Possi alikuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Uchukuzi.

**C: Uteuzi wa Katibu Tawala wa Mkoa na Naibu Makatibu Wakuu**

1. CP. Salum Hamduni ameteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga. Kabla ya uteuzi huu, CP. Hamduni alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), anachukua nafasi ya Prof. Siza Tumbo ambaye amerejea Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA);

2. Bw. Ismail Rumatila ameteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Afya. Kabla ya uteuzi huu, Bw. Rumatila alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA);

3. Bw. Atupele Webster Mwambene ameteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anayeshughulikia masuala ya elimu. Kabla ya uteuzi huu, Bw. Mwambene alikuwa Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;

4. Bw. Abdul Rajab Mhinte ameteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia mifugo. Kabla ya uteuzi huu, Bw. Mhinte alikuwa Afisa Mwandamizi, Ofisi ya Rais – Ikulu; na

5. Bw. Methusela Stephen Ntonda ameteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Kabla ya uteuzi huu, Bw. Ntonda alikuwa Afisa Mwandamizi, Ofisi ya Rais – Ikulu.

**D: Uhamisho wa Naibu Makatibu Wakuu**

1. Dkt. Grace Elias Magembe amehamishwa kutoka Wizara ya Afya kwenda kuwa Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anayeshughulikia masuala ya afya;

2. Dkt. Charles Enock Msonde amehamishwa kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwenda kuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Ujenzi;

2

3. Dkt. Wilson Mahera Charles amehamishwa kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwenda kuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia anayeshughulikia masuala ya elimu ya msingi na sekondari;

4. Prof. Daniel Elius Mushi amehamishwa kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwenda kuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia anayeshughulikia masuala ya sayansi na elimu ya juu;

5. Dkt. Franklin Jasson Rwezimula amehamishwa kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwenda kuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria;

6. Dkt. Khatibu Malimi Kazungu amehamishwa kutoka Wizara ya Katiba na Sheria kwenda kuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati anayeshughulikia masuala ya umeme na nishati jadidifu.

   Aidha, Dkt. James Peter Mataragio atakuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati anayeshughulikia masuala ya petroli na gesi;

7. Bw. Ludovick James Nduhiye amehamishwa kutoka Wizara ya Ujenzi kwenda kuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Uchukuzi;

8. Dkt. Suleiman Hassan Serera amehamishwa kutoka Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwenda kuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Kilimo anayeshughulikia masuala ya ushirika na umwagiliaji.

   Aidha, Dkt. Hussein Mohamed Omar atakuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Kilimo anayeshughulikia masuala ya maendeleo ya mazao na usalama wa chakula.

**E: Uhamisho wa Wakuu wa Wilaya**

1. Kanali Maulid Hassan Surumbu amehamishwa kutoka Wilaya ya Tarime kwenda kuwa Mkuu wa Wilaya ya Mbarali. Kanali Sulumbu anachukua nafasi ya Brigedia Jenerali Denis Filangali Mwila ambaye amepangiwa majukumu mengine;

2. Meja Edward Flowin Gowele amehamishwa kutoka Wilaya ya Rufiji kwenda kuwa Mkuu wa Wilaya ya Tarime;

3. Bw. James Wilbert Kaji amehamishwa kutoka Wilaya ya Tanga kwenda kuwa Mkuu wa Wilaya ya Moshi;

4. Bw. Zephania Stephan Sumaye amehamishwa kutoka Wilaya ya Moshi kwenda kuwa Mkuu wa Wilaya ya Lushoto;

3

5. Bw. Japhari Kubecha Mghamba amehamishwa kutoka Wilaya ya Lushoto kwenda kuwa Mkuu wa Wilaya ya Tanga;

6. Bi. Rebecca Sanga Msemwa amehamishwa kutoka Wilaya ya Morogoro kwenda kuwa Mkuu wa Wilaya ya Bahi;

7. Bi. Gift Isaya Msuya amehamishwa kutoka Wilaya ya Bahi kwenda kuwa Mkuu wa Wilaya ya Pangani; na

8. Bw. Mussa Ramadhani Kilakala amehamishwa kutoka Wilaya Pangani kwenda kuwa Mkuu wa Wilaya ya Morogoro.

**F: Uteuzi wa Katibu Tawala wa Wilaya**

1. Bi. Proscovia Jaka Mwambi ameteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Bukoba.

**G: Uhamisho wa Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri**

1. Bw. John Lipes Kayombo amehamishwa kutoka Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwenda kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Jiji la Arusha;

2. Bw. Juma Hamsini Seph amehamishwa kutoka Halmashauri ya Jiji la Arusha kwenda kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Jiji la Tanga;

3. Bw. Fredrick Damas Sagamiko amehamishwa kutoka Halmashauri ya Jiji la Tanga kwenda kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma;

4. Bw. Elihuruma Mabelya amehamishwa kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kwenda kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam;

5. Bw. Jomary Mrisho Satura amehamishwa kutoka Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwenda kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke;

6. Bi. Joanfaith John Kataraia amehamishwa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro kwenda kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida;

7. Bw. Jeshi Godfrey Lupembe amehamishwa kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Singida kwenda kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro;

8. Bw. Khamis Jaaphar Katimba amehamishwa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Msalala kwenda kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi;

9. Bi. Rose Robert Manumba amehamishwa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi kwenda kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Msalala;

10. Bw. Stephen Edward Katemba amehamishwa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kwenda kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali;

11. Bw. Missana Kalela Kwangura amehamishwa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kwenda kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga;

12. Bi. Happines Joachim Msanga amehamishwa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba kwenda kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe; na

13. Dkt. Amon David Mkoga amehamishwa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe kwenda kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba.

**H: Uteuzi wa Wakuu wa Taasisi**

1. Bw. Crispin Chalamila ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Kabla ya uteuzi huu, Bw. Chalamila alikuwa Afisa Mwandamizi, Ofisi ya Rais – Ikulu;

2. CPA. Moremi Andrea Marwa ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL). Kabla ya uteuzi huu, CPA. Marwa alikuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Magereza (SHIMA); na

3. Dkt. Irene Isaka ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Aidha, uapisho wa Mawaziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wakili Mkuu wa Serikali, Jaji wa Mahakama ya Rufani, Katibu Tawala wa Mkoa na Naibu Makatibu Wakuu wateule utafanyika Ikulu – Dar es Salaam kesho tarehe 15 Agosti, 2024 saa 8.00 mchana.

Sharifa B. Nyanga
Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

# Waziri Prof. Kabudi: Tuna Deni Kubwa kwa Watanzania



*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi (Mb) akizungumza na wajumbe wa menejimenti ya Taasisi zilizo chini ya Wizara yake mara baada ya kuapishwa Ikulu Jijini Dar es Salaam.*

Tuna deni kubwa kwa watanzania wa kawaida la kuwahudumia na kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Hayo yameelezwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Palamaghamba Kabudi (Mb) alipowasili katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, baada ya kuapishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Ikulu jijini Dar es Salaam kushika nafasi hiyo.

"Tuna deni kubwa kwa watanzania wa kawaida katika Sekta ya Sheria ambapo tumepewa dhamana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhudumia wananchi kwa kuwa kazi ya kuongoza nchi siyo kazi

ndogo na wanasheria tuna nafasi kubwa ya kulifanya taifa lisimame au lidondoke, tunatakiwa kusaidia mhimili wa Mahakama," alisema Prof. Kabudi.

Aliongeza kuwa tumepewa jukumu kubwa la kumsaidia Mhe. Rais Dkt. Samia kutoa huduma kwa wananchi ambapo tunatakiwa kutimiza wajibu wetu kwa mujibu wa Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunamshukuru Mhe. Rais Dkt. Samia kwa hisani aliyotupa kututeua katika nafasi mbali mbali za Sekta ya Sheria na kutupa dhamana hii. pamoja na Prof. Kabudi, viongozi wengine wa Sekta ya Sheria walioteuliwa na kuapishwa na Mhe. Rais Dkt. Samia ni pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dkt. Franklin Rwezimula, Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Saleh Possi, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Samwel Maneno na Jaji wa Mahakama ya Rufani, Mhe. Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi.

Pia, amewashukuru na kuwapongeza viongozi wote waliohudumu katika nafasi mbali mbali kwa kazi kubwa waliyoifanya ambapo nafasi hizo wamepewa wengine na viongozi hao ni Dkt. Boniphace Luhende aliyekuwa Wakili Mkuu wa Serikali na Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na sasa Jaji wa Mahakama ya Rufani.

Hafla hiyo ya ukaribisho baada ya uapisho imehudhuriwa na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mhe. Jumanne Sagini, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Eliakim Maswi, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo, baadhi ya viongozi wa Wizara hiyo na taasisi zake, Menejimenti na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Jummanne Sagini akizungumza na Viongozi wa Wizara na Taasisi zilizoko chini ya Wizara hiyo baada ya kuwakaribisha na kuwapokea Viongozi wa Wizara na Taasisi zake walioteuliwa na kuapishwa Ikulu Jijini Dar es Salaam.*



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akimsikiliza kwa makini Mhe. Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi wakati akizungumza na viongozi wa Wizara na taasisi zilizoko chini ya Wizara hiyo baada ya kuapishwa Ikulu Jijini Dar es Salaam.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria ndugu Eliakim Maswi akizungumza wakati akiwakaribisha viongozi wa Wizara hiyo walioteuliwa baada ya viongozi hao kuapishwa Ikulu Jijini Dar es Salaam.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akizungumza na wajumbe wa menejimenti ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria baada ya ukaribisho uliyofanyika Jijini Dar es Salaam*



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi (aliyekaa katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo baada ya ukaribisho uliyofanyika kwenye Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Jijini Dar es Salaam.*

# Waziri Dkt. Balozi Pindi Chana Aongoza Mapokezi ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria



*Katibu Mkuu wa Katiba na Sheria ndugu Eliakimu Maswi akipokea ua la ukaribisho kutoka kwa Mhasibu Mwandamizi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Chiku Liundi, alipowasili Ofisini hapo baada ya hafla ya uapisho iliyofanyika Ikulu Jijini Dar es Salaam.*

Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana amewaongoza Viongozi wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara hiyo na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kumpokea na kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria ndugu Eliakim Maswi kwa kuteuliwa na kuapishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza baada ya hafla ya uapisho uliofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam, Mhe Balozi Dkt. Pindi Chana amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumteua ndugu Maswi kushika nafasi hiyo kwa kuwa ni mtu mwenye uzoefu na maarifa hivyo ataiwezesha Wizara ya Katiba na Sheria kuendelea kupiga hatua katika kuliletea taifa maendeleo.

Akizungumza wakati wa mapokezi hayo Mhe. Chana amemuelezea ndugu Maswi kama mtu mchapakazi na mwenye uzoefu wa muda mrefu katika utumishi wa umma kwa kuwa amewahi

kushika nyadhifa mbalimbali serikalini huku akiahidi kumpa ushirikiano mkubwa ili kwa pamoja waweze kumsaidia Mhe. Rais Dkt. Samia kuwaletea wananchi maendeleo.

Akimkaribisha kiongozi huyo Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini amemkaribisha Maswi kwenye familia ya Wizara ya Katiba na Sheria ili kuendelea kushirikiana vyema kutekeleza majukumu ya Wizara hiyo ikiwa ni sehemu ya kuendeleza kazi kubwa iliyofanywa na mtangulizi wake Bi. Mary Makondo aliyeteuliwa na Mhe. Rais Dkt. Samia kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma.

Mhe. Sagini amemuelezea ndugu Maswi kama mtu shupavu anayefanya kazi kwa bidii bila kuchoka usiku na mchana huku akiweka wazi kuwa anayo furaha kubwa kumpongeza kwa dhati kuteuliwa na kuapishwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria huku akibainisha kuwa kuteuliwa kwake ni ishara na imani kubwa aliyonayo kwake Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na uwezo wake wa kuleta mabadiliko chanya katika Wizara hii muhimu nchini.

“Nina imani kubwa kuwa uongozi wako utaendelea kuimarisha utendaji wa Wizara na kuleta mabadiliko chanya katika Sekta ya Sheria, tunaahidi kukupa ushirikiano" alisema Mhe. Sagini.

Akiongea mbele ya Waziri wa Katiba na Sheria na viongozi walioko chini ya Wizara hiyo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi amesema kuwa amefanya kazi na Maswi wakati akiwa kiongozi katika nafasi mbalimbali na kueleza kuwa anamtambua kama kiongozi anaye jitolea katika kuhakikisha utawala bora na uimarishaji wa Sekta ya Sheria na kusisitiza kuwa anaamini kuwa chini ya uongozi wake wananchi watashuhudia maboresho makubwa na mafanikio katika nyanja mbalimbali za Sekta ya Sheria nchini.

Naye Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Luhende akimpongeza kiongozi huyo kwa kuteuliwa kushika nafasi hiyo muhimu ametumia nafasi hiyo kumuelezea kiongozi huyo majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambayo ni kuendesha, kuratibu na kusimamia mashauri yote ya madai, usuluhishi, katiba, haki za binadamu na uchaguzi yanayofunguliwa na Serikali au dhidi ya Serikali ndani na nje ya nchi. Dkt. Luhende ameahidi kumpa ushirikiano kiongozi huyo na kumtakia kila la heri katika majukumu yake mapya huku akimuomba kuendelea na moyo wa kujituma kwa maendeleo ya taifa letu.

Akizungumza mara baada ya kukaribishwa na viongozi hao Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria ndugu Eliakim Maswi amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hasaan kwa Imani kubwa aliyonayo kwake na kuamua kumteua katika nafasi hiyo huku akiomba viongozi hao kufanya kazi kwa bidii na ushirikiano kwa kuwa wote wanafanya kazi ya kujenga nyumba moja.

Ndugu Eliakim Maswi aliteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria tarehe 21 Julai, 2024. Kabla ya Uteuzi huo ndugu Maswi alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA).



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, ndugu Eliakim Maswi akizungumza na Viongozi wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo baada ya kuapishwa Ikulu na kupokelewa kwenye ukumbi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam.*



*Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi akizungumza na viongozi wa Wizara ya Katiba na Sheria wakati wa hafla ya kumpokea Katibu Mkuu wa Wizara hiyo ndugu Eliakim Maswi (hayupo pichani) iliyofanyika katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam.*



*Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Luhende akizungumza na viongozi wa Wizara ya Katiba na Sheria wakati wa hafla ya kumpokea Katibu Mkuu wa Wizara hiyo ndugu Eliakim Maswi (hayupo pichani) iliyofanyika katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam.*



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Pindi Chana (aliyesimama katikati) akiwa na baadhi ya Viongozi wa Taasisi za Wizara hiyo na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya hafla ya kumpokea Katibu Mkuu ndugu Eliakim Maswi jijini Dar es Salaam.*



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (aliyesimama kushoto) akipokea nyaraka za makabidhiano kutoka kwa aliyekuwa Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende baada ya kukabidhiwa Ofisi kwenye hafla iliyofanyika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Jijini Dar es Salaam.*

# Wakili Mkuu wa Serikali Akabidhiwa Ofisi

Wakili Mkuu wa Serikali akabidhiwa Ofisi rasmi tarehe 19 Agosti, 2024 baada ya kuteuliwa na kuapishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Wakili Mkuu wa Serikali na kuapishwa tarehe 15 Agosti, 2024 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

"Wewe ni mtangulizi wangu, uliwahi kuongoza Ofisi hii kipindi kilichopita ukiwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali na sasa umerejea kuongoza Ofisi hii ukiwa Wakili Mkuu wa Serikali, hapa ni nyumbani, Ofisi hii unaifahamu, nikupongeze kwa kuteuliwa na kuaminiwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kushika nafasi hii, nami niko tayari kukupa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yako,"

amesema Dkt. Luhende.

Katika makabidhiano hayo, Dkt. Luhende alimkabidhi Dkt. Possi nyaraka mbali mbali za uendeshaji wa Ofisi ikiwemo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ni sheria mama ya nchi na taarifa ya mashauri yanayoendeshwa na Ofisi hii ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo ya uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi ya ndani na nje ya nchi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake.

Akipokea nyaraka hizo, Dkt. Possi alimshukuru Dkt. Luhende kwa makabidhiano ya Ofisi ili aweze kuendelea kutekeleza majukumu ya Ofisi kwa mujibu wa dhamana waliyokasimiwa na Serikali na amemshukuru Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumuamini na kumteua kushika nafasi hiyo na yuko tayari kushirikiana na Menejimenti ya Ofisi hiyo, watumishi na wadau kutekeleza majukumu ya Ofisi kwa niaba ya Serikali katika kuhudumia wananchi.

Makabidhiano hayo yameshuhudiwa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo ambaye amewapongeza viongozi hao na kuwatakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu kwa kila mmoja kwa nafasi yake katika kuendeleza gurudumu la maendeleo.



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (Wa kwanza kushoto) na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo mara baada ya kukabidhiwa Ofisi na aliyekuwa Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende. Makabidhiano hayo yamefanyika kwenye Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Jijini Dar es Salaam.*



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akizungumza na baadhi ya viongozi wa Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) (ambao hawapo pichani) walipotembelea Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa lengo la kujitambulisha Ofisi kwake jijini Dar es Salaam.*

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Kuendeleza Ushirikiano na TLS

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itaendelea kushirikiana na Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS) kwa lengo la kuendelea kuisaidia Serikali kutekeleza majukumu yake kwa kuangalia namna gani itatumia taaluma ya sheria kwa maslahi ya Taifa ili kuvutia wawekezaji wa sekta mbalimbali nchini.

Hayo yamesemwa leo na Wakili Mkuu wa Serikali wakati akizungumza na Rais wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS) na ujumbe wake katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika kwenye ukumbi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam.

Dkt. Possi amesema kuwa maeneo ambayo wamepanga

kushirikiana ni kukuza taaluma ya sheria kwa wanasheria ambao wamesoma na kuhitimu kwa kuendelea kuwajengea uwezo katika nyanja mbalimbali ili waweze kutumia vyema taaluma ya sheria kulinda rasilimali za nchi kwa kusimamia vyema Sekta ya Sheria ili kuendelea kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji nchini.

Ameeleza kuwa hivi sasa dunia imebadilika kwa kuwa tuna wawekezaji wa kimataifa wanaokuja kuwekeza Tanzania na pia wapo wawekezaji wetu ambao wanakwenda kuwekeza nje ya Tanzania hivyo kwa kuwajengea uwezo mawakili wetu kutasaidia wawekezaji hawa kuhudumiwa na watanzania ndani na nje ya nchi hivyo kusaidia kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

"Sisi hatutaki mwekezaji anayetoka nje ya Tanzania atumie mwanasheria wa kigeni, wanasheria wa Tanzania wapo, Shule ya Sheria kwa Vitendo ipo na inatoa wahitimu wanasheria ambao ni watanzania", amesema Dkt. Possi.

Akizungumza kuhusu umuhimu wa kutunza maadili kwa mawakili nchini Dkt. Possi amesema kuwa tunajukumu muhimu la kutunza maadili ya mawakili waliopo na wanaokuja na kutambua umuhimu wa kazi yetu, hii itasaidia kujenga uaminifu na kukuza thamani yetu kwa wananchi tunaowahudumia.

Aidha, Dkt. Possi amewataka viongozi wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS) waendelee kuishauri Serikali kuhusu namna inavyoweza kuboresha shauri mbalimbali zilizopo ili kusaidia kuendana na wakati tuliopo kwa lengo la kusaidia kulinda rasilimali za nchi kwa manufaa ya wananchi wote.

Dkt. Possi ametumia mkutano huo kukipongeza Chama cha Mawakili wa Serikali (PBA) na TLS kwa kuingia makubaliano ya kushirikiana katika maeneo mbalimbali huku akiahidi kusimamia mashirikiano hayo ili kuhakikisha wanaimarisha Sekta ya Sheria nchini.

Naye, Rais wa TLS ndugu Boniphace Mwabukusi akizungumza katika kikao hicho ameiomba Serikali kuendelea kuwapa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yao huku akiweka wazi kuwa tayari wamekubaliana na Chama cha Mawakili wa Serikali kushirikiana katika masuala mbalimbali ambayo yatasaidia kuendeleza Sekta ya Sheria nchini.



*Rais wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS) ndugu Boniphace Mwabukusi akizungumza na wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (hawapo pichani) alipowatembelea kwa lengo la kujitambulisha kwao jijini Dar es Salaam.*

> ***"Sisi hatutaki mwekezaji anayetoka nje ya Tanzania atumie mwasheria wa kigeni, wanasheria wa Tanzania wapo, Shule ya Sheria kwa Vitendo ipo na inatoa wahitimu wanasheria ambao ni watanzania", amesema Dkt. Possi.***



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akitoa salamu za Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa kikao cha Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Ally Possi na Baraza la Uongozi la Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) walipotembelea Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa lengo la kujitambulisha jijini Dar es Salaam.*




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (aliyesimama kulia) akimkabidhi Jarida la Wakili Mkuu Rais wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS) ndugu Boniphace Mwabukusi alipomtembelea kwa lengo la kujitambulisha Ofisini kwake jijini Dar es Salaam.*



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akiongoza kikao kati ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na wajumbe wa Baraza la Uongozi wa TLS walipotembelea kwa lengo la kujitambulisha jijini Dar es Salaam.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akizungumza na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Mbeya, Mhe. Joachim Tiganga wakati wa ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Mbeya.*

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yatoa Ushirikiano Uendeshaji Mashauri ya Serikali Mbeya

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imepongezwa na Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Mbeya kwa ushirikiano katika uendeshaji mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake.

Hayo yameelezwa na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Mbeya, Mhe. Joachim Tiganga wakati wa ziara ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo alipofika Ofisini kwake wakati wa ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoa wa Mbeya.

"Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoa wa Mbeya inatupa ushirikiano wa kutosha katika uendeshaji wa mashauri ya Serikali Mbeya kwa kuwa Mkoa huu una mashauri mengi ukilinganisha na mikoa mingine ambapo baadhi ya mashauri yana maslahi mapana kwa taifa hivyo Mahakama kwa kushirikiana na Ofisi hii tunapenda kuendesha mashauri na kuyamaliza kwa wakati," amesema Mhe. Jaji Mfawidhi Tiganga.

Naye Bi. Mtulo amesema kuwa lengo la ziara hiyo ni kukagua utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoa wa Mbeya, kuonana na wadau na kufahamu masuala yanayohitaji kufanyiwa kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uendeshaji wa mashauri.

Akiwasilisha taarifa ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Mbeya, Wakili wa Serikali Mfawidhi, Allan Shija alisema kuwa tangu kuanzishwa kwa Ofisi ya Mbeya mwaka 2018, jumla ya mashauri 361 yaliendeshwa, mashauri 259 yalimalizika na 102 yanaendelea ambapo asilimia 40 ni mashauri ya ardhi, 38% ya madai, 15% mashauri ya maombi mbalimbali (Applications), 4% mashauri ya kazi, na 3% ya mashauri ya maombi ya gharama. Aliongeza kuwa kati ya mashauri hayo 102, mashauri 74 yapo Mahakama Kuu ya Tanzania, 24 Mahakama ya Rufani, mashauri mawili (02) yapo Tume ya Usuluhishi na Upatanishi, shauri moja (01) lipo Mahakama ya Wilaya ya Mbeya na lingine moja (01) lipo Mahakama ya Wilaya Tunduma.



*Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Mbeya, Mhe. Joachim Tiganga akimkaribisha Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo Ofisini alipofika kukagua utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Jijini Mbeya.*



*Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Mbeya, Mhe. Joachim Tiganga akizungumza na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo (hayupo pichani) Ofisini kwake wakati wa ziara ya kukagua utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Mbeya.*



*Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Mbeya, Mhe. Aisha Sinda akimkaribisha Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo (kulia) Ofisini kwake alipofika kumtembelea wakati wa ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Mbeya.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo (wa tatu kulia) akiwa kwenye picha ya pamoja na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Mbeya, Mhe. Joachim Tiganga (wa tatu kushoto) baada ya kikao Ofisini kwake wakati wa ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Mbeya.*

# Menejimenti ya OWMS Yatakiwa Kuongeza Ushirikiano Katika Kutekeleza Majukumu Yake



*Wakili MKuu wa Serikali Dkt. Ally Possi akizungumza na Wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (hawapo pichani) wakati wa kikao cha kutoa mwelekeo wa Ofisi hiyo kilichofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Ofisi hiyo Jijini Dar es Salaam.*

Wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wametakiwa kutekeleza majukumu yao kwa kushirikiana hatua itakayowasaidia kutekeleza majukumu yao kwa wakati ili kufikia malengo yao waliyojiwekea ndani ya muda ulipangwa.

Wito huo umetolewa na Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi wakati wa kikao cha kwanza cha Menejimenti tangu alipoteuliwa kushika nafasi hiyo na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kilicholenga kufahamiana na kutoa mwelekeo wa utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku kilichofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Ofisi hiyo Jijini Dar es Salaam.

Ameongeza kuwa kufanya kazi kwa ushirikiano kutawasaidia viongozi hao kuwa na mtazamo wa pamoja katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku hasa jukumu mama la kusimamia, kuratibu na kuendesha mashauri yote ya madai na usuluhishi yaliyopo katika mahakama na mabaraza mbalimbali nchini na hatimaye kuisaidia Ofisi hii kupata ushindi mara mashauri hayo yanapomalizika.

Dkt. Possi ameeleza kuwa kufanya kazi kwa ushirikiano

ni muhimu kwa kuwa kutawasaidia viongozi wa Ofisi hiyo kuongeza ujuzi, uzoefu na kuwa na mtazamo chanya wa pamoja na kuongeza ubunifu utakao saidia kupata suluhisho sahihi katika kukabiliana na changamoto zilizopo.

Katika hatua nyingine, Dkt. Possi amewataka viongozi hao kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuwa wepesi wa kutoa ushauri wenye tija ili kwa pamoja kama viongozi waweze kusaidia kusukuma mbele gurudumu la maendeleo.

Aidha, amewasihi viongozi hao kuendelea kuwasimamia vyema watumishi walioko chini yao ikiwa ni pamoja na kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili sambamba na kujali maslahi yao ya kiutumishi ili watumishi hao waweze kutekeleza majukumu yao kwa wakati.

Dkt. Possi amewasisitiza wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa kufuata Sheria, taratibu na kanuni za kudumu za utumishi wa umma kwa kuwa kufanya kazi kwa kufuata sheria, taratibu, na kanuni za utumishi wa umma ni msingi wa utoaji wa huduma bora kwa wananchi na kuhakikisha kwamba utumishi wa umma unafanyika kwa njia ya uwazi, uadilifu na uwajibikaji wakati wote wawapo ndani na nje ya kituo cha kazi.

Naye, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Alice Mtulo akizungumza na wajumbe hao wakati akisoma taarifa ya utekelezaji ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ameahidi kumpa ushirikiano Dkt. Possi pamoja na kufanyia kazi maelekezo na miongozo yote atakayoitoa kwa lengo la kuhakikisha wanamsaidia Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwaletea wananchi maendeleo.



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akisoma taarifa ya utekelezaji ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa kikao cha Menejimenti kilichofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Ofisi hiyo Jijini Dar es Salaam.*



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (aliyeketi katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya kikao kilichofanyika jijini Dar es Salaam.*

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yapongezwa Songea



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akisaini kitabu cha wageni alipofika Ofisini kwa Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Songea, Mhe. James Karayemaha (hayupo pichani) wakati wa ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Songea.*



*Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Songea, Mhe. James Karayemaha akizungumza na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo (hayupo pichani) wakati wa ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Songea.*

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imepongezwa kwa utendaji kazi mzuri na kwa ushirikiano katika kuhakikisha kuwa kesi zote zinaendeshwa vizuri kwa kufuata sera ya Mahakama ya kufanya Usuluhishi katika mashauri ambayo yanaweza kuisha kwa usuluhishi mkoani Ruvuma.

Hayo yameelezwa na Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Songea, Mhe. James Karayemaha wakati akizungumza na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo alipofika Ofisini kwake mahakamani wakati wa ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Songea na mahusiano baina ya Ofisi hiyo na wadau mbalimbali ikiwemo Mahakama.

Ameongeza kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Songea inashirikiana na Mahakama kutoa elimu ya sheria kwa jamii kupitia redio na mabanda ya maonesho na wakati wote Mawakili wa Ofisi hii wanafika mahakamani kwa wakati.

Naye Bi. Mtulo aliishukuru Mahakama kwa ushirikiano wanaowapatia Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Songea na kupelekea kutekeleza majukumu yao kwa amani na weledi zaidi.

Pia, Bi. Mtulo alionana na Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, ndugu Joel Mbewa na kumshukuru kwa ushirikiano na kuiongezea Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Songea vyumba vya Ofisi ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu.

Akitoa taarifa ya utendaji kazi kwa Bi. Mtulo, Wakili wa Serikali Mfawidhi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Songea, ndugu Egidy Mkolwe amesema kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu Serikali Songea imeendelea kuiwakilisha Serikali mahakamani na katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika mashauri yote yanayofunguliwa na au dhidi ya Serikali katika mkoa huo. Bi. Mtulo alitoa rai kwa watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Songea kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi kwa maslahi mapana ya Taifa letu.




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo (aliyesimama Katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, ndugu Joel Mbewa (wa pili kulia) alipofika Ofisini kujitambulisha wakati wa ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Songea.*



*Wakili wa Serikali Mfawidhi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Songea, Egidy Mkolwe akiwasilisha taarifa ya utendaji kazi kwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo (aliyeketi mbele) wakati wa ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Songea.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akizungumza na Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Joel Mbewa alipofika Ofisini kwake kujitambulisha wakati wa ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Songea.*




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo (aliyesimama katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Joel Mbewa (wa pili kulia) alipofika Ofisini kwake kujitambulisha wakati wa ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Songea.*

# Suma JKT Yatakiwa Kuongeza Kasi Mradi wa Ujenzi Jengo la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Alice Mtulo akizungumza wakati wa kikao cha kamati ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wakili Mkuu kilichofanyika katika Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma.*

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo ameitaka kampuni ya Suma JKT ambayo inaendelea na ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuongeza kasi na kutoa taarifa ya utekelezaji wa mradi kila wiki hatua itakayosaidia kutatua changamoto za ujenzi wanazokutana nazo ili kukamilisha mradi huo kwa wakati.

Bi. Mtulo ameyasema hayo alipotembelea mradi huo na kushiriki kikao cha kamati ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kilichofanyika Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma.

Akizungumza katika kikao hicho Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Alice Mtulo amemtaka mkandarasi huyo siyo tu kuongeza kasi ya ujenzi wa mradi huo pia amemuelekezakuhakikisha anajenga jengo hilo kwa ubora ili litakapokamilika liendane na thamani ya fedha zilizotumika

kukamilisha ujenzi huo.

Amemhimiza mkandarasi kufanya kazi kwa pamoja na mshauri mwelekezi huku akitoa wito kwa mkandarasi huyo kuhakikisha anakuwa na vikao vya mara kwa mara, kutoa taarifa za utekelezaji wa mradi kwa kila wiki ili taarifa hizo zisaidie kutatua changamoto zinazojitokeza kwa wakati.

Bi. Mtulo amemuagiza mkandarasi kuendelea kuzingatia usalama mahali pa kazi kwa wafanyakazi wanaojenga jengo hilo ikiwemo kupewa vifaa na elimu ya kujilinda dhidi ya majanga yanayoweza kutokea wakati wote wanapoendelea na kazi katika eneo la mradi.

Kwa upande wake Mkadiriaji Majenzi wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ndugu Daniel Nkruma ameahidi kuendelea kutoa ushauri wenye tija na kwa wakati hatua itakayosaidia mkandarasi na mshitiri wa mradi kushirikiana kwa pamoja kutoa rasilimali zinazotakiwa kwa wakati ili kazi hiyo iweze kumalizika ndani ya muda uliopangwa.

Naye Meneja Mradi wa Suma JKT, Kanali Saul Chiwanga ameahidi kufanyia kazi changamoto zote zilizoanishwa wakati wa kikao hicho ili kuhakikisha anaongeza kasi ya ujenzi wa mradi na kuweza kukamilisha azma ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha taasisi zote zinahamia Dodoma.

Kikao cha Kamati ya Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni mwendelezo wa vikao vya ufuatiliaji wa ujenzi kwa kila mwezi vyenye lengo la kuhakikisha vinamsimamia mkandarasi ili aweze kufanya kazi kwa ufanisi na kukamilisha kazi ya ujenzi wa jengo hilo kwa wakati.



*Meneja Mradi wa Suma JKT, Kanali Saul Chiwanga akitoa taarifa ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa kikao cha Kamati ya Ujenzi kilichofanyika Mtumba Jijini Dodoma.*



*Wajumbe wa Kamati ya Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo (hayupo pichani) wakati akizungumza na wajumbe hao wakati wa Kikao cha Kamati hiyo Mtumba Jijini Dodoma.*

# Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Atembelea Maonesho ya Sabasaba




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo (aliyesimama katikati) akiwa na watumishi wa Ofisi ya wakili Mkuu wa Serikali alipotembelea banda la Ofisi hiyo kwenye Maonesho ya Sabasaba jijini Dar es Salaam.*

Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Sekta ya Sheria nchini itaendelea kutoa elimu na msaada wa kisheria kwa wananchi wa rika zote ili kuhakikisha kila mwanachi anafahamu haki na wajibu wake katika kuiletea nchi yetu maendeleo.

Haya yamezungumzwa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Alice Mtulo alipotembelea Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa "Sabasaba" ili kujionea bidhaa mbalimbali zinazopatikana katika maonesho hayo.

Bi. Mtulo amesema kuwa uwepo wa Maonesho ya Sabasaba ni fursa nzuri kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala mbalimbali ya kisheria, haki za wananchi na jinsi ya kufuata sheria kwa kufanya hivi kutasaidia kuongeza uelewa wa masuala ya sheria kwa jamii hatua itakayosaidia kujenga jamii imara inayozingatia sheria.

Ameongeza kuwa kupitia maonesho hayo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inasaidia kukuza ufahamu wa huduma za kisheria nchini kwa wananchi wengi hasa wale wa daraja la chini ambao wengi wao hawana uelewa wa kutosha kuhusu masuala ya kisheria pamoja na huduma zinazotolewa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Hivyo, maonesho haya yatasaidia kuwapa nafasi wananchi wengi kufahamu huduma za sheria zinazopatikana na jinsi wanavyoweza kuzifikia kwa urahisi.

Alifafanua kuwa, kupitia maonesho hayo Ofisi kwa kushirikiana na wadau wote walioko chini ya Wizara ya Katiba na Sheria watatoa

ushauri wa kisheria kwa wafanyabiashara na washiriki wengine wa maonesho ili kusaidia kutatua migogoro ya kisheria wanayokumbana nayo katika shughuli zao za kilimo na biashara hususan masuala ya kodi.

Aidha, alifafanua kuwa kupitia Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itaendelea kujenga mahusiano mazuri na Wadau mbalimbali kwa kuzingatia ukweli kuwa maonesho ya Sabasaba huvutia wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi pamoja na serikali, sekta binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali na wananchi katika kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati kwa wananchi wote.

Alieleza kuwa uwepo wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika maonesho haya kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuhamasisha wananchi kufuata misingi ya sheria katika shughuli zao za kila siku kwa kutoa taarifa na elimu juu ya sheria zinazohusu kilimo, ardhi, na biashara kwa kuwa kupitia maonesho haya Ofisi itahamasisha wafanyabiashara kote nchini kufuata sheria na kanuni za biashara ili kuhakikisha wafanyabiashara na wanachi kwa ujumla wanafuata sheria wakati wote.

Bi. Mtulo alihitimisha ziara yake kwa kusema kuwa ushiriki wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika maonesho ya Sabasaba kwa mwaka huu ni muhimu kwa kuwa Ofisi yake itahakikisha wananchi wanapata elimu, ushauri na msaada wa kisheria ili kuboresha maisha yao na shughuli zao za kila siku katika kujiletea maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa yalifanyika kuanzia tarehe 28 Juni, 2024 na kuhitimishwa tarehe 13 Julai, 2024 ambapo yalifunguliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akipokea zawadi ya jarida na vipeperushi kutoka kwa Afisa Uhusiano Mwandamizi wa EWURA Bi. Asiatu Msuya mara baada ya kutembelea banda la Ofisi hiyo kwenye Maonesho ya Sabasaba jijini Dar es Salaam.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akitazama moja ya bidhaa inayopatikana ndani ya banda la Zanzibar alipotembelea banda hilo kwenye Maonesho ya Sabasaba jijini Dar es Salaam.*

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yashiriki Maonesho ya 48 ya Sabasaba




*Kaimu Mkurugenzi Idara ya Usimamizi wa Mashauri na Udhibiti Ubora wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Camilius Ruhinda (wa kwanza kulia) akifafanua jambo kwa mzee Hussen Ally alipotembelea banda la maonesho la Ofisi hiyo wakati wa Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) jijini Dar es Salaam.*

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeshiriki Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa yaliyofanyika kuanzia tarehe 28 Juni, 2024 katika Viwanja vya Sabasaba Jijini Dar es Salaam na yanayohitimishwa tarehe 13 Julai, 2024 yakiwa na kauli mbiu isemayo, ***"Tanzania: Mahali Sahihi Pa Biashara na Uwekezaji"***.

Akizungumza wakati wa maonesho hayo, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Mashauri na Udhibiti Ubora, Camilius Ruhinda amesema kuwa lengo la kushiriki Maonesho hayo ni kuwajengea wananchi uelewa na kutoa elimu kuhusu majukumu yanayotekelezwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambayo ni kusimamia, kuratibu na kuendesha mashauri yote ya Madai, Usuluhishi, Katiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi.

Ameongeza kuwa ushiriki wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika maonesho hayo utasaidia kwa kiasi kikubwa kujitangaza na kufahamika kwa wadau na wananchi zaidi tofauti na sasa ambapo majukumu hayo yamekuwa yakichanganywa na yale ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Ruhinda amezitaja faida nyingine kuwa ni kutoa huduma

za kisheria bila malipo kwa watu wenye uwezo mdogo kifedha ambao hawawezi kumudu gharama za Mawakili na gharama nyingine za kisheria, pamoja na ushauri wa kisheria, msaada wa kisheria katika kufahamu uelekeo wa kesi na msaada wa kuandaa nyaraka za kisheria kwa ufasaha.

Ruhinda alifafanua kuwa ushiriki huu unalenga kutoa elimu na ushauri wa kisheria kwa wajasiriamali na wafanyabiashara kwa kuwa Maonesho ya SabaSaba ni jukwaa kubwa linalovutia wafanyabiashara kutoka katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Alisisitiza kuwa wanatoa elimu ya kisheria kwa kuzingatia ukweli kuwa wengi wa wafanyabiashara wanaoshiriki maonesho hayo wanakabiliwa na changamoto mbalimbali za kisheria zinazoweza kuathiri uendeshaji wa biashara zao. Hivyo kwa kutoa elimu kuhusu sheria zinazohusu biashara, mikataba na masuala mengine muhimu ya kisheria, Ofisi hii inawasaidia wajasiriamali kuelewa haki na wajibu wao, hivyo kuzuia changamoto za kisheria ili kuwasaidia kufanya maamuzi bora kwa ajili ya biashara zao na nchi kwa ujumla.

Aidha, Ruhinda alieleza kuwa ushiriki wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika maonesho haya unalenga kuhamasisha ufuataji wa sheria za biashara, kwa kutoa mwongozo na taarifa muhimu kuhusu sheria na kanuni, ili kuhakikisha kuwa biashara zinaendeshwa kwa kufuata taratibu sahihi, hivyo kuimarisha mazingira ya kibiashara nchini.

Alifafanua kuwa kwa kufanya hivi itasaidia kuongeza uwazi, uwajibikaji na uaminifu katika shughuli za kibiashara, jambo ambalo ni muhimu kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi.

Akizitaja faida nyingine za kushiriki maonesho haya, Ruhinda aliongeza kuwa Ofisi hii inatumia maonesho ya SabaSaba kukuza uelewa wa haki za kibiashara miongoni mwa wajasiriamali kwa kuwa wengi wao hawana uelewa wa kutosha kuhusu haki zao kisheria, ambazo ni elimu kuhusu haki za miliki na usajili wa alama za biashara.

“Kupitia maonesho haya, Ofisi inatoa mafunzo na ushauri kuhusu haki hizi, hivyo kuwawezesha wajasiriamali kutambua na kulinda haki zao”, alisema Ruhinda.

Akizungumzia fursa zinazopatikana kupitia maonesho hayo, Ruhinda alisema kuwa kupitia maonesho ya Saba Saba Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itaweza kujenga mahusiano na wadau mbalimbali wa biashara ikiwa ni pamoja na taasisi za serikali, sekta binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali.

Alisema kuwa ushiriki huu unalenga kuimarisha ushirikiano katika masuala mbalimbali ya kisheria na biashara, hivyo kuchangia katika kuboresha mazingira ya kibiashara na kukuza uchumi wa taifa.

Amewakaribisha wananchi na viongozi mbalimbali wa Serikali, sekta binafsi, wananchi na wadau wote kutembelea banda la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali lililopo ndani ya Banda la Mahakama ya Tanzania mkabala na Banda la JKT.



*Mzee Sebastian Kingu akisaini kitabu cha wageni alipotembelea Banda la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) yanayoendelea jijini Dar es Salaam.*

# Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Atembelea Maonesho ya Nanenane



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akisaini kitabu cha wageni alipotembelea Banda la Maonesho la Ofisi Wakili Mkuu Serikali kwenye maonesho ya Nanenane mkoani Dodoma. Waliosimama nyuma yake ni watumishi wa Ofisi hiyo.*

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo ametembelea Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi "Nanenane' kwa lengo la kujionea huduma mbalimbali zinazotolewa na taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa zinazoshiriki maonesho hayo kwa lengo la kuunga mkono juhudi za Serikali kuwaletea wananchi maendeleo.

Akizungumza baada ya kuwasili katika banda la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Mtulo amesema kuwa kupitia maonesho haya Mawakili wa Serikali watapata fursa ya kutoa elimu ya msaada wa kisheria kwa wananchi wanaotembelea maonesho hayo kwa kuwa ushiriki wa Maonesho ya Nane Nane ni fursa nzuri kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala mbalimbali ya kisheria, ili kuwawezesha wananchi kufahamu haki zao.

Ameongeza kuwa ushiriki wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwenye maonesho

haya kutaisaidia Ofisi kujenga mahusiano na wadau mbalimbali wanaofanya kazi na Ofisi hii kwa kuwa maonesho haya ni moja ya jukwaa linalowavutia wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi.

Aidha, Bi. Mtulo amesema kuwa kupitia maonesho haya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itashirikiana na wadau wengine kuendelea kutoa ushauri mbalimbali kuhusu msaada wa kisheria hususan kwa wakulima, wavuvi na wafugaji ambao ndio walengwa haswa wa maonesho haya ili kusaidia kutatua changamoto mbalimbali za kisheria wanazokumbana nazo kila siku katika kutekeleza shughuli zao za kila siku.

Bi. Mtulo ameeleza kuwa Mawakili wa Serikali watapata fursa ya kuendelea kuhamasisha umuhimu wa wananchi kufanya majukumu yao kwa kufuata misingi ya sheria kwa kuendelea kutoa elimu juu ya sheria zinazohusu masuala mbalimbali kama vile kilimo, ardhi na biashara ili wananchi waweze kufahamu sheria, miongozo na kanuni zinazohusu Sekta ya Kilimo, Uvuvi na ufugaji ili kupunguza migogoro inayoweza kujitokeza katika jamii na kuathiri shughuli za maendeleo katika jamii.

Bi. Mtulo ameendelea kufafanua kuwa kupitia maonesho haya Ofisi yake itaendelea kujitangaza kwa wananchi na wadau wake ili kukuza ufahamu kuhusu majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa wananchi ambayo ni kusimamia, kuratibu na kuendesha mashauri yote ya madai, usuluhishi, katiba, haki za binadamu na uchaguzi yanayofunguliwa na serikali au dhidi yake katika Mahakama na mabaraza mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Maonesho ya Nanenane mwaka 2024 yalifanyika tarehe 01 Agosti, 2024 na kufungwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 8 Agosti 2024 katika viwanja vya Nanenane mkoani Dodoma yakiwa yamebeba kauli mbiu isemayo “Chagua Viongozi Bora wa Serikali za Mtaa kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.”



*Katibu Mkuu wa Wizara ya katiba na Sheria ndugu Eliakim Maswi akisaini kitabu cha wageni alipotembelea Banda la Maonesho la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwenye maonesho ya Nanenane Jijini Dodoma. Aliyesimama nyuma kushoto ni Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo.*




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo (aliyeketi) akipata maelezo kuhusu namna Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inavyotekeleza majukumu yake kutoka kwa watumishi wa Ofisi hiyo alipotembelea Banda la Ofisi hiyo kwenye maonesho ya Nanenane Jijini Dodoma.*



# Wanafunzi wa Mafunzo kwa Vitendo Watakiwa Kufanya Kazi kwa Kutunza Siri za Serikali

Wanafunzi wa mafunzo kwa vitendo wametakiwa kutekeleza majukumu yao kwa kufuata sheria na taratibu pamoja na kutunza siri kuhusu taarifa zote watakazofanyia kazi wakati wote watakapokuwa wakitekeleza majukumu yao kwa ajili ya kujifunza na kupata uzoefu kwa vitendo.

Wito huo umetolewa na Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Mashauri na Udhibiti Ubora ndugu Camilius Ruhinda wakati wa kikao kwa ajili ya kutoa maelekezo kwa wanafunzi wa mafunzo kwa vitendo (interns) kutoka vyuo mbalimbali nchini kuhusu mambo muhimu ya kufuatwa katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam.

Kiongozi huyo ameongeza kuwa ili wanafunzi hao waweze kujifunza vyema kwa vitendo kwa muda wote watakaokuwa Ofisini hapo, wanafunzi hao wanapaswa kuwa waaminifu kufanya kazi kwa ushirikiano, uwazi, na uwajibikaji ili waweze kujenga msingi mzuri wa taaluma zao.

Ameendelea kueleza kuwa kujifunza kwa bidii na juhudi kwa kuonyesha weledi katika kila jambo watakalofanya kutawawezesha kufanya vizuri katika ajira na kazi za kujitegemea huko mbeleni pindi watakapohitimu masomo yao.

Aidha, ndugu Ruhinda amewataka wanafunzi hao kuendelea kujifunza kuhusu masuala yanayohusu kada zao pasipo kuchoka hatua itakayowasaidia kuongeza ujuzi na maarifa yao ya kitaaluma kwa vitendo na kushiriki kwenda mahakamani na vikao vinavyohusu uendeshaji wa mashauri.

Ndugu Ruhinda amewasihi wanafunzi hao kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa kushirikiana wao kwa wao na watumishi wote

wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuomba msaada pale wanapokwama na kuuliza maswali kwa wenzao, viongozi wao watumishi wote kwa lengo la kupata uelewa pale wanapokutana na changamoto.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, ndugu Adam Nyando amewataka wanafunzi hao kuwa nadhifu wakati wote wanapokuwa kazini kwa kuvaa mavazi yenye staha yanayokubalika kwenye utumishi wa umma pamoja na kufika mapema kazini ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa wakati.

Ameongeza kuwa wanafunzi hao wanapaswa kujiepusha na migogoro mahala pa kazi kwa kipindi chote watakachokuwa Ofisini hapo na badala yake wafanye kazi kwa ushirikiano ili kuleta tija katika utekelezaji wa majukumu yao.

Naye, Wakili wa Serikali Mwandamizi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Magdalena Makabungu amewaasa wanafunzi hao kuzingatia maelekezo watakayopewa na wasimamizi wao ili waweze kusimamia vyema majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali hatua itakayosaidia kujenga msingi bora katika masuala yote yanayohusu taaluma ya sheria na kada nyingine kwa manufaa ya taifa kwa ujumla.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi hao wa Shule ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo Bi. Shangwe Simba wameshukuru Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuwapokea na kuwapa miongozo ambayo itawasaidia kujifunza na kupata uzoefu kutoka kwa watumishi wa Ofisi hiyo waliobobea katika fani mbalimbali ikiwemo Sheria, TEHAMA, Ugavi, Uhasibu na Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu hatua itakayowajengea msingi bora ili waweze kuwa watumishi bora wa umma wa baadaye.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imepokea wanafunzi 45 wa mafunzo kwa vitendo kutoka vyuo mbalimbali nchini ambapo wanafunzi wa kada ya sheria ni 28 na wanafunzi wa kada nyingine ni 17.



*Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Mashauri na Udhibiti Ubora wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Camilius Ruhinda akizungumza na wanafunzi wa mafunzo kwa vitendo kuhusu taratibu za Ofisi hiyo wakati wa kikao cha kuwakaribisha wanafunzi hao kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Ofisi hiyo jijini Dar es Salaam.*

# Wakili wa Serikali Apata Tuzo ya Utatuzi wa Migogoro kwa Njia ya Usuluhisi



*Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma (aliyeketi katikati) akiwa katika picha ya pamoja na wadau mbalimbali waliokabidhiwa tuzo kwa mchango mkubwa katika kuimarisha usuluhishi. Wa pili kutoka kushoto (waliosimama) ni ndugu Hangi Chang'a, Mkurugenzi Msaidizi wa Mashauri ya Kikatiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.*

Wakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Francis Wisdom Oswald amepata tuzo maalum ya utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi kwa kutambua mchango na juhudi zake zilizochangia kuongezeka kwa kiwango cha mafanikio ya upatanishi katika mashauri ya kisheria kwa mwaka 2023. Tuzo hiyo imetolewa kwa baadhi ya wadau waliotoa mchango mkubwa katika kuimarisha usuluhishi.

Tuzo hiyo yenye maneno yasemayo, ***"This Award is given to Francis Wisdom State Attorney in Recognition of Exceptional Improving the Success Rate of Mediation 2023,"*** ambayo kwa kiswahili ina maanisha kuwa, "Tuzo hii imetolewa kwa ndugu Francis Wisdom Oswald, Wakili wa Serikali kwa kuthamini mchango wa kipekee wa uboreshaji wa kiwango cha upatanishi 2023."

Tuzo hiyo ilitolewa na Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Juma ambaye alikuwa Mgeni Rasmi ambayo ilifanyika

kwenye ukumbi wa Mwalimu Nyerere International Convention Centre ambapo tuzo hiyo ilipokelewa kwa niaba yake na ndugu Hangi Chang'a, Mkurugenzi Msaidizi wa Mashauri ya Kikatiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Hafla ya kutambua mchango wa wadau katika kufanikisha utatuzi wa migogoro mbalimbali kwa njia ya usuluhishi iliandaliwa na Mahakama ya Tanzania kwa lengo la kuthamini na kusherehekea juhudi za wadau katika Sekta ya Sheria ambao wamechangia kwa kiwango kikubwa kupunguza mzigo wa mashauri mahakamani.

Hafla hiyo imehudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Mahakama, Mawakili wa Serikali na wadau wa usuluhishi. Hafla hiyo yenye kauli mbiu isemayo, ***"Umuhimu wa Utatuzi wa Migogoro kwa Njia ya Usuluhishi katika Kukuza Uchumi Endelevu: Wajibu wa Mahakama na Wadau,"*** ililenga kuthamini na kusherehekea juhudi za wadau katika Sekta ya Sheria ambao wamechangia kwa kiwango kikubwa kupunguza mzigo wa mashauri mahakamani.

Katika hafla hiyo, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilishiriki na kutoa mchango wake ambapo masuala mbali mbali yalitiliwa mkazo ikiwemo umuhimu wa kutumia njia za usuluhishi katika kutatua migogoro ili kuimarisha amani na kuleta ufanisi katika mfumo wa haki nchini Tanzania.

Pia, hafla hiyo ilitanguliwa na mjadala ulioendeshwa na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mheshimiwa Zahra Maruma ambao ulijikita kwenye mada isemayo, "Kwa Nini Sio Upatanishi," ambapo washiriki walipata fursa ya kujadiliana, kubadilishana mawazo na uzoefu katika kusimamia, kuendesha na kuratibu mashauri ya usuluhishi nchini. Pia, walibadilishana mawazo kuhusu faida za usuluhishi katika kusaidia upatikanaji wa haki kwa haraka na kwa njia isiyo ya mvutano.

Wakili Oswald aliishukuru Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kutengeneza mazingira bora ya kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya usuluhishi na aliwapongeza viongozi wa Ofisi hiyo pamoja na watumishi wote kwa ushirikiano wao katika kuhakikisha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inapiga hatua katika uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi.

Pia, aliongeza kuwa anaishukuru Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kumuamini na kumpa dhamana kubwa ya kusimamia mashauri kwa niaba ya Serikali na taasisi zake ambayo imefanya aonekane na kutambuliwa katika kutoa mchango mkubwa wa kufanikisha utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi.



*Wakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Francis Wisdom (pichani), atunukiwa Tuzo ya Utatuzi wa Migogoro kwa Njia ya Usuluhishi kwa mwaka 2023 na Mahakama ya Tanzania.*

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yaibuka Kidedea Mchezo wa Kuvuta Kamba

Timu ya Wanaume wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeibuka na ushindi wa kishindo baada ya kuibwaga timu ya kuvuta kamba ya wanaume wa Hospitali ya Mwananyamala katika mchezo uliofanyika kwenye viwanja vya Chuo cha Ustawi wa Jamii Jijini Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Mwenyekiti wa muda wa michezo wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ndugu Athumani Zunda amesema ushiriki wao katika bonanza la michezo la Wiki ya Hospitali ya Mwananyamala mbali ya kuwa limesaidia kwa kiasi kikubwa kuitangaza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, pia ni kutekeleza kwa vitendo agizo la Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kasim Majaliwa Majaliwa (Mb) linalotaka taasisi za umma kuanzisha vikundi vya michezo na mazoezi kwa watumishi wake ili kuepukana na magonjwa yasiyo ambukiza.

Timu ya kuvuta kamba ya wanaume ya Wakili Mkuu wa Serikali ilidhihirisha nguvu, umoja, na ustadi wa hali ya juu katika mchezo wa kuvuta kamba kwa kuibuka mshindi dhidi ya timu ya wanaume ya Hospitali ya Mwananyamala ambapo ilifanikiwa kuwavuta katika mizunguko yote miwili na kufanikiwa kupata medali za ushindi walizokabidhiwa na Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mwananyamala Dkt. Zavery Benela.

Mchezo wa kuvuta kamba kati ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Hospitali ya Mwananyamala ulikuwa na msisimko mkubwa uliovutia watazamaji wengi wakiwemo wafanyakazi wa taasisi mbalimbali zilizoshiriki tamasha hili pamoja na wakazi wa maeneo ya jirani.

Zunda ameongeza kuwa mashindano hayo pia wameyatumia kama sehemu ya kujiandaa kwa ajili ya kujiweka vizuri na Mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI), yanayotarajiwa kufanyika baadaye mwaka huu mkoani Morogoro.

Zunda aliongeza kuwa tamasha hili ni fursa nzuri kwa wananchi na watumishi wa Serikali wa rika zote kuungana pamoja kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kujifunza umuhimu wa kufanya mazoezi kama njia mojawapo ya kuzuia magonjwa yasiyoambukiza kama vile kisukari, shinikizo la damu, na magonjwa ya moyo ambayo katika siku za hivi karibuni yamekuwa tishio kwa watu mbalimbali hasa vijana na hivyo kupunguza nguvukazi ya Taifa.

Aidha, ameishukuru Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano waliotoa kwa timu hiyo kwa kuiwezesha timu hiyo kushiriki mazoezi ipasavyo na kushiriki mashindano hayo kikamilifu na kuchangia kwa kiasi kikubwa kuongeza chachu kwa wachezaji hao na hatimaye kufanikisha ushindi wa kishindo uliopatikana katika mchezo huo.

Uzinduzi wa Tamasha la Wiki ya Mwananyamala Hospitali ulikwenda sambamba na Uzinduzi wa Bonanza la Michezo Mwananyamala lilihusisha utoaji wa huduma za vipimo bila malipo, elimu ya afya pamoja na mashindano ya michezo kwa taasisi za umma lilianza tarehe 27 Julai, 2024 hadi tarehe 3 Agosti, 2024.

JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA
**OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI**

**OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI**
**10 Barabara ya Kivukoni**
**S. L. P 71554**
**11101 DAR ES SALAAM**

**Simu: +255 22 2127384**
**Fax: +255 22 2127385**
**Nukushi: www.osg.go.tz**
**Barua pepe: info@osg.go.tz**

## ANUANI ZA POSTA NA MAENEO ZILIPO OFISI ZA WAKILI MKUU WA SERIKALI MIKOANI

| | |
|---|---|
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1902<br>41218 DODOMA<br>Jengo la Katiba na Sheria (UDOM)<br>Barua pepe: dodoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 130<br>31101 MUSOMA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mara@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1280<br>63114 MTWARA<br>Maadili House<br>Barua pepe: mtwara@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 394<br>33101 MWANZA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mwanza@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 595<br>51108 IRINGA<br>Lilokuwa jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Iringa<br>Barua pepe: iringa@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 106<br>35102 BUKOBA<br>Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Mhakiki Mali<br>Barua pepe: kagera@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 564<br>57101 SONGEA<br>Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: ruvuma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 43<br>37101 SHINYANGA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: shinyanga@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 60<br>21101 TANGA<br>Jengo la Mkonge<br>Barua pepe: tanga@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 119<br>45112 TABORA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: tabora@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 202<br>25101 MOSHI<br>Jengo la TRA Moshi<br>Barua pepe: kilimanjaro@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 690<br>55103 SUMBAWANGA, Mtaa wa Ukaguzi<br>Jengo la Ukaguzi, Gorofa ya pili<br>Barua pepe: rukwa@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 66<br>23101 ARUSHA<br>Jengo la AICC, Arusha<br>Barua pepe: arusha@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 710<br>53107 MBEYA<br>Jengo la Madini<br>Barua pepe: mbeya@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 172<br>47101 KIGOMA, Jengo la NHC, Ghorofa ya Pili,<br>Kiwanja Na. 148 & 149, Mtaa wa Lumumba.<br>Barua pepe: kigoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>Jengo la NSSF, Ghorofa la Nne<br>MOROGORO, Barabara ya zamani DSM<br>Barua pepe: morogoro@osg.go.tz |